

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE

Simu Na. 023 32935403 (BaruazoteziandikwekwaMkurugenziMtendaji)

Nakishi.023 32935402

E - MAIL:

Ded@chaliz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)

S.L.P. 65,

**CHALINZE**

**KUMB.NA.CHAL/LD/2584**

**08/7/2022**

Mkurugenzi Mkuu,  
Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC),  
S.L.P 938,  
**DAR ES SALAAM.**

**YAH: UTAMBULISHO WA MMILIKI WA KIWANJA NAMBA 12 KITALU "B"  
VIGWAZA CHALINZE**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

Tunapenda kukujulisha kuwa tulipokea barua ambayo haikuwa na kumbukumbu namba ya tarehe 05.07.2022 kutoka kwa ndugu **ATHUMANI OMARY SAIDI** akitufahamisha kuwa aliuza eneo lake ambalo alilipata kutoka kwa wamiliki wa asili katika kijiji cha Vigwaza; akalipanga, akalipima na kuuza kiwanja tajwa hapo juu kwa wawekezaji wajulikanao "**UNION MEAT ABATTOIRS COMPANY LIMITED**" wa S.L.P 9104, Dar es Salaam iliyosajiliwa na Brela kwa namba **155567481**.

Aidha nakujulisha kuwa eneo lenye ukubwa wa **mita za mraba 36,321** tumelikagua kwa kushirikiana na Mtendaji wa kijiji husika na hatukubainisha mgogoro wowote wakati wa ukaguzi.

Kwa sababu hiyo nawaleta kwako **UNION MEAT ABATTOIRS COMPANY LIMITED** kwa hatua zaidi za **umilikishaji wa kiwanja hiki kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za umilikishaji wa maeneo ya uwekezaji**.

Nakutakia utekelezaji mwema.

Ramadhani Possi  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**CHALINZE**



**Nakala kwa:**

1. Kamishna wa Ardhi Msaidizi,  
Mkoa wa Pwani,  
1 MTAA WA ARDHI,  
S. L. P 9230,  
**11477, DAR ES SALAAM –(kwa taarifa)**
  
2. Mkurugenzi Mkuu,  
UNION MEAT ABATTOIRS LIMITED,  
S.L.P 9104,  
**DAR ES SALAAM- (kwa ufuatiliaji na ufuatiliaji).**
  
3. Athumani Omary Saidi,  
S.L.P 30298,  
**KIBAHA –(kwa taarifa na ufuatiliaji)**



Faint signature or handwritten text, possibly a name, located at the bottom center of the page.